**TAMKO KUHUSU KITENDO CHA JESHI LA POLISI KUWANYIMA DHAMANA GODLISTEN MALISA NA BONIFACE JACOB KINYUME NA TARATIBU ZA KISHERIA**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesikitishwa na kitendo cha Jeshi la Polisi kuwanyima dhamana Godlisten Malisa na ndugu Boniface Jacob. Ndugu Godlisten Malisa ni Mwanaharakati na Mkurugenzi wa Shirika la Haki Foundation ambalo limekuwa likisaidia watu wengi hapa nchini wenye changamoto mbalimbali kupata misaada mbalimbali. Tarehe 13 Aprili 2024 kupitia kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii ndugu Malisa na Jacob walitoa taarifa za kupotea kwa ndugu Robert Mushi (Babu G) na hatimae Jeshi la Polisi kutoa taarifa kwa vyombo vya habari kuwa maiti yake ipo katika hospitali ya Polisi Kilwa Road, Dar es Salaam.

Tarehe 23 Aprili 2024, Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam Jumanne Muliro alitoa taarifa kwa vyombo vya habari na kuwatuhumu ndugu Malisa na Jacob kuwa walitoa taarifa za uongo na uzushi. Kufuatia taarifa hiyo, Jeshi la Polisi lilitoa wito kwa ndugu Malisa na Jacob kufika katika kituo cha Polisi kati Dar es Salaam. Baada ya kuitika wito huo alihamisi tarehe 25 Aprili, ndugu Malisa na Jacob walikamatwa na kutokupewa dhamana kwa mujibu wa Sheria. Kifungu cha 32 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinaeleza wazi kwamba mtuhumiwa akikamatwa anapaswa kuachiwa kwa dhamana au kufikishwa Mahakamani ndani ya saa 24, kinyume na hapo ni ukiukwaji wa Katiba na Sheria za nchi.

Kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kila mtu ana haki na uhuru wa kutoa maoni au taarifa kwa njia yoyote atakayoichagua. Haki hii inalindwa pia na Mikataba mbalimbali ambayo Tanzania imeridhia. THRDC tunaamini kwamba watanzania wana haki ya kuhoji kupitia mitandao au kutoa taarifa kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea katika jamii na kufanya hivyo sio kosa kwa mujibu wa Sheria.

**Wito wetu**

- Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unasikitishwa na kitendo cha Jeshi la Polisi kuwanyima dhamana ndugu Malisa na Jacob kinyume na Sheria, huu ni ukiukwaji wa haki za watuhumiwa. Hivyo, tunalisihi Jeshi la Polisi kuwaachia kwa dhamana.
- Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unatoa wito kwa Jeshi la Polisi kuwaacha watanzania watumie uhuru wao kuhoji kupitia mitandao au kutoa taarifa kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea katika jamii.
- Mtandao unatoa wito kwa jeshi la Polisi kufanya upelelezi kwa kuzingatia Sheria na Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO). Watuhumiwa hawapaswi kukaa kwenye vituo vya Polisi kwa muda mrefu nje ya muda wa kisheria na pia upelelezi unapaswa kufanyika kabla ya watuhumiwa kukamatwa.
- Bado tunaendelea kudai mabadiliko ya sheria ya makosa ya kimtandao kwani imegeuka kuwa shubiri na kutumika vibaya kukamata na kubinya uhuru wa watanzanaia kutumia mitandao kukosoa, kuhoji na kutetea haki za binadamu. Sheria hii inachangamoto nyingi ikiwemo kuwapa polisi mamlaka ya kuchukua vifaa vya mawasiliano vya watuhumiwa na kuingilia faragha za wananchi kinyume na sheria za ulinzi wa taarifa na faragha.

**Imetolewa na,**

**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC),**

**Aprili 27, 2024 Dar es Salaam, Tanzania.**